Nilimjia Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- naye akiwa anapiga mswaki kwa mswaki wa mti mbichi, Akasema: na ncha ya mswaki ikiwa katika ulimi wake, naye akisema: AAGH, AAGH (sauti ya kujigogoa), na mswaki ukiwa mdomoni mwake, kana kwamba anajigogoa

Kutoka kwa Abuu Musa Al-Ash'ariy -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- Amesema: (Nilimjia Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- naye akiwa anapiga mswaki kwa mswaki wa mti mbichi, Akasema: na ncha ya mswaki ikiwa katika ulimi wake, naye akisema: AAGH,AAGH (sauti ya kujigogoa), na mswaki ukiwa mdomoni mwake, kana kwamba anajigogoa).

[Sahihi] [Wamekubaliana Bukhaariy na Muslim]

Anaeleza Abuu Musa Al Ash'ariy -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake-: yakuwa yeye alikuja kwa Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- naye akipiga mswaki kwa kutumia mti mbichi kwasababu husafisha kikamilifu na hausambaratiki mdomoni; ukakera, na hakika alikuwa kaweka mswaki juu ya ulimi wake, mpaka akawa kana kwamba anajitapisha.

http://www.sunnah.global/hadeeth/sw/show/3456